**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WAZARA YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI, KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Ofisi ya Bunge
**DODOMA.**

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WAZARA YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI, KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, katika wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema (Mb), napenda kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo mwaka wa fedha 2019/2020.

2. **Mheshimiwa Spika**, Ninasoma hotuba hii kwa niaba ya msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kufuatia adhabu ya Bunge hili kwake, dhidi ya maoni yake aliyotoa Bungeni, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaamini kwamba, maoni yake yalipaswa kulindwa chini ya Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunamtakia kila la kheri na vilevile tunamkumbusha Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema kwamba mapambano ya haki dhidi ya utawala wa sheria yanaendelea.

3. **Mheshimiwa Spika**, tunawatia moyo Viongozi wakuu wa CHADEMA wanaokabiliwa na kesi katika mahakama mbalimbali nchini, wakiongozwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe na viongozi wengine waandamizi. Tunawaombea na kuwatia moyo kwa kauli mbiu ya kwamba kesho ni Imara kuliko jana.

4. **[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**
Aidha katika kipindi hiki, Sheria za Tanzania ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na sheria mbalimbali za nchi na kanuni zinavunjwa hadharani, huku kauli za kuwatisha wananchi kupigwa hadi kuchakaa, kinyume na sheria za nchi hii zikitamalaki; na sasa katika mitaa mbalimbali ya viunga vya Jiji la Dodoma kauli za "**Tutawapiga hadi wachakae"** zimekuwa ni vibwagizo vinavyokwenda sambamba na Hotuba za Viongozi wa Serikali, ni kipindi ambacho matamko yasiyozingatia tena Katiba, Sheria na Kanuni yanatolewa hadharani, tena na viongozi,

miongoni mwao wakiwa na wajibu wa kutekeleza majukumu ya kuhakikisha usalama wa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mali zao zinakuwa salama. Ni kipindi ambacho mamlaka za ulinzi sasa zinasimama kwenye majukwaa ya kisiasa kama wanasiasa wengine bila kuzingatia matakwa ya sheria zetu.

**B. POLISI KUPUUZA MISINGI YA KATIBA NA SHERIA DHIDI YA VYAMA VYA SIASA NCHINI:**

**5. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya awamu ya tano ilikuja na zuio la mikutano ya hadhara ambalo kila mmoja anajua linakiuka Sheria ya Vyama vya Siasa ambavyo vina haki kikatiba na kisheria ya kufanya kazi za siasa ikiwa ni pamoja na mikutano na maandamano.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

**13. Mheshimiwa Spika**, Mathalani Jeshi la Polisi Mkoani Mwanza lilifikia hatua ya kuwakataza wafuasi na wanachama wa CHADEMA kushiriki misiba wakiwa na sare za chama au bendera. Aidha, marufuku hiyo pia ilihusu kutofanya vikao vyao vya kikatiba vya ndani, Bendera za CHADEMA nazo zinashushwa kwa amri za viongozi wa Serikali, Mjini Makambako na sasa Wilayani Arumeru Serikali kupitia Mkuu wa Wilaya ya Arumeru imeelekeza marufuku ya kupeperusha kwa bendera za CHADEMA, hizi ni amri zinatolewa na serikali na zitatekelezwa na Jeshi la Polisi, Ukiukwaji huu mkubwa wa sheria na serikali inamfumbia macho mpaka leo ni kuiweka amani ya Taifa hili rehani.

**14. Mheshimiwa Spika**, tarehe 17 Aprili, 2018 baadhi ya Viongozi wa Baraza la Wazee wa CHADEMA walikamatwa na Jeshi la Polisi Mkoani Morogoro usiku wa manane wakiwa wamepumzika na kupelekwa Kituo Kikuu cha Polisi cha Mkoa bila kuelezwa kosa lao wala sababu za wao kuvamiwa na kusweka rumande.

**15. Mheshimiwa Spika**, baada ya Jeshi la Polisi kukaa na viongozi hao kwa muda zaidi ya masaa kumi waliachiwa bila masharti yoyote kwa maelekezo kuwa wakiwahitaji watawapigia simu. Huu ni udhalilishaji mkubwa ambao unafanyika katika nchi yetu.

**16. Mheshimiwa Spika**, Aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na sasa mwanachama wa Chama cha ACT Wazalendo, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad alipokuwa na ziara yake Pemba, wanachama na wapenzi wa demokrasia walizuiwa kumpokea katika Uwanja wa Ndege, aidha kwa nyakati mbalimbali Jeshi la Polisi limezuia mara kadhaa Chama cha ACT Wazalendo kutembelea Mikoa ya Lindi na Tanga ambapo Chama hicho kilitarajia kufanya shughuli zake za kisiasa.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

## C. HAKI ZA KIRAIA NA VIFO VINAVYOTOKANA NA UKATILI WA JESHI LA POLISI

**19. Mheshimiwa Spika,** Tunayo nafasi finyu katika hotuba hii ya kueleza matukio ya ukatili wa polisi dhidi ya raia wa nchi hii. Tunasisitiza kuwa Katiba yetu inaruhusu mfumo wa Vyama vingi vya Siasa na sheria zetu zinatoa haki na wajibu kwa vyama hivyo katika kuendesha shughuli zao za kisiasa nchini. Haki ya kujumuika na haki ya kujiunga na chama chochote au taasisi nyingine yoyote zinajumuishwa na kuitwa haki za kiraia hivyo kuwapa mateso mpaka vifo watu wote ambao kwa namna moja ama nyingine wanahusiana na Vyama vya Siasa vya Upinzani sio tu kumkosea Mwenyezi Mungu bali ni kukiuka haki ambazo sisi wenyewe tumezikubali kama Taifa.

**20. Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa tarehe 17 Februari, 2018 ulifanyika uchaguzi wa marudio katika majimbo ya Kinondoni na Siha na baadhi ya Kata nchini. Ikumbukwe kuwa uchaguzi wowote unatoa wajibu na haki kwa Vyama vya Siasa vinavyoshiriki uchaguzi.

**21. Mheshimiwa Spika**, Moja ya haki za Vyama na Wagombea wanaoshiriki uchaguzi ni pamoja na haki ya kuwa na Mawakala katika kila kituo cha uchaguzi na pia wakala wa ziada kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi. Katika hali ya kushangaza mpaka kufikia tarehe 16 Februari, 2018 majira ya jioni Mawakala wa CHADEMA walikuwa hawajapewa viapo vyao vya Uwakala pamoja na kuwa ni takwa la kisheria viapo hivyo kutolewa siku saba kabla ya uchaguzi.

**22. Mheshimiwa Spika**, Tume ya Uchaguzi kupitia kwa Mkurugenzi wake waliahidi kutoa viapo hivyo kabla ya siku ya uchaguzi jambo ambalo halikutekelezwa. Ulikuwa ni uamuzi wa busara wa mtu yeyote au kiongozi kuhakikisha kuwa Mawakala wake wanakuwa na viapo pamoja na barua za utambulisho wa kuwaruhusu kuingia vituoni.

**23. Mheshimiwa Spika**, Kwa kauli za Jeshi la Polisi ni kuwa maandamano ni kosa la jinai na hata kusema neno maandamano kwa sasa inaonekana ni kosa la jinai huku wakijua ni haki ya kikatiba na kisheria. Viongozi wa Chama waliondoka pamoja na wanachama ambao ni Mawakala kwenda kudai viapo na barua za utambulisho kwa ajili ya usimamizi wa kura, ilikuwa ni lazima kulingana na muda pamoja na uhitaji kwani wasingefanya hivyo vituo vyote vingekosa Mawakala.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

## D. JESHI LA POLISI NA UKIUKWAJI WA SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI

**29. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi linatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria ya Jeshi la Polisi na Watoa Huduma Wasaidizi wa Polisi ikiwa ni pamoja na Kanuni za Kudumu za Polisi. Aidha kwa upande mwingine wa kusimamia na kuratibu masuala ya uhalifu nchini, Jeshi la Polisi linatumia na linatakiwa kuongozwa na sheria ya Kanuni za Adhabu pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

**30. Mheshimiwa Spika,** Ni kwa msingi huo ibara ya 13(6)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapiga marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo. Pamoja na msingi na takwa hili la kikatiba vituo vingi vya polisi nchini vimegeuka sehemu za kutweza utu na kutesa raia badala ya lengo la msingi la ulinzi na usalama wa raia wa Jeshi hilo.

**31. Mheshimiwa Spika**, ni hivi majuzi tu Mkoani Mbeya ambapo kijana Allen Mapunda (20) mkazi wa Iyela alifariki muda mfupi baada ya kuachiwa na Jeshi la Polisi, pamoja na Polisi Mkoa wa

Mbeya kukanusha kuhusika na kifo hicho lakini mtu yeyote anaweza kuhoji ushahidi wa kimazingira baada ya kijana huyo kuachiwa na Jeshi la Polisi kuwa huenda akawa amepigwa na kutweza jambo lililopelekea kifo chake na ndiyo maana Polisi baada ya kuona udhaifu wa mtuhumiwa wakaamua kumwachia huru kukwepa lawama.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

**33. Mheshimiwa Spika**, tarehe 22 Machi, 2018 Kituo cha Polisi cha Mwandoya Wilayani Meatu kilichomwa moto na wananchi wenye hasira kali baada ya kupewa taarifa kuwa mmoja wa mwananchi mwenzao aliuwawa katika kituo hicho akiwa mikononi mwa Polisi.

**34. Mheshimiwa Spika**, katika hali kama hii ambayo wananchi wanajichukulia sheria mkononi baada ya kukosa imani na vyombo vilivyopewa mamlaka ya kusimamia na kutekeleza sheria kuwa sehemu ya kukiuka sheria husika, hakika mustakabali wa amani na utulivu wa nchi yetu utakuwa mashakani. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Jeshi la Polisi na Polisi wote kwa ujumla kuwa hata kama mfumo wa ndani ya nchi unawalinda kwa ukiukwaji wa Katiba na haki za binadamu bado kuna jumuiya za kimataifa ambapo Tanzania imeridhia mikataba yake ambazo zinaweza kuchukua hatua.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

## E. UKIUKWAJI WA HAKI ZA MAHABUSU KATIKA VITUO VYA POLISI

**36. Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 23 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinamtaka askari au mtu yeyote anayemkamata mtuhumiwa kumjulisha makosa yake, sio lazima iwe katika lugha ya kitaalam lakini ni haki ya mtuhumiwa kujulishwa makosa yake hata kwa lugha ya kawaida ili ajue sababu za yeye kukamatwa.

**37. Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na utaratibu ambao umeanza kuzoeleka katika utendaji wa Jeshi la Polisi ambapo watuhumiwa wamekuwa wakikamatwa bila kujulishwa makosa yao jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya sheria. Mawakili au ndugu wa watuhumiwa wanapojaribu kuhoji ni kwa nini

watuhumiwa wanashikiliwa bila kuelezwa makosa yao wanajibiwa kuwa wanasubiri maelekezo kutoka juu.

**38. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata kauli ya serikali kuwa huko juu ni wapi? Hayo mamlaka mengine ya "amri kutoka juu" ambayo hayajatajwa na sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai ni yapi? Kwa nini Jeshi la Polisi limerekebisha sheria bila kuletwa Bungeni kwa kutengeneza mamlaka zingine ambazo sio kwa mujibu wa sheria?

**39. Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 32 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinatoa masharti na utaratibu kwa Jeshi la Polisi kumfikisha Mahakamani mtuhumiwa yeyote ndani ya masaa 24 isipokuwa kwa makosa ambayo adhabu yake ni kifo. Masharti haya yamekuwa kiini macho katika Vituo vingi vya Polisi nchi ambapo Jeshi la Polisi limekuwa likiwashikilia watuhumiwa zaidi ya masaa ambayo yanatakiwa kwa mujibu wa sheria.

**40. Mheshimiwa Spika**, imekuwa ni kawaida kwa Wanachama na Viongozi wa Vyama vya Upinzani kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu bila kupelekwa Mahakamani. Jeshi la Polisi linapotakiwa kutoa maelezo kwa nini hawawapeleki watuhumiwa Mahakamani wanarudia kauli ile ile ya "tunasubiri maelekezo kutoka juu".

**41. Mheshimiwa Spika**, adha ya ukiukwaji huu wa sheria sio tu kwa Wanasiasa wa Vyama vya Upinzani tu bali imeenda hata kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu ambapo ni majuzi tu ambapo Mwenyekiti wa Mtandao wa Wanafunzi wa Elimu ya Juu Abdul Nondo alikaa kwenye mahabusu za Polisi Iringa na Dar es Salaam kwa zaidi ya siku 15 bila kupelekwa Mahakamani kinyume na utaratibu wa kisheria.

**42. Mheshimiwa Spika**, wapo baadhi ya watu ambao wameshikiliwa kwenye Vituo vya Polisi mbalimbali kwa zaidi ya miezi miwili bila kupelekwa Mahakamani, aidha wapo makumi na mamia ya wananchi ambao wamekuwa wakiteseka kwenye vituo mbalimbali vya Polisi kwa muda mrefu kinyume na utaratibu wa sheria kwa tuhuma za makosa ya kimtandao. Kasi ya wananchi kukamatwa kwa makosa yanayodaiwa ni ya mtandao imekuwa kubwa katika serikali hii ya awamu ya tano ambayo ni ishara ya kuminywa kwa uhuru wa mawazo na uhuru kupokea na kutoa habari.

**43. Mheshimiwa Spika**, Katika randama ya Wizara Fungu 28 ukurasa 5 inaonyesha kuwa jumla ya makosa 2,571 ya mtandao yaliripotiwa kufikia Februari, 2018. Pamoja na takwimu hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoji kuwa pamoja ubovu wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ambayo kimsingi inatakiwa kufutwa kabisa, hakuna kifungu chochote cha sheria hiyo ambacho kinawapa Jeshi la Polisi mamlaka ya kuwashikilia watuhumiwa wa makosa hayo kwa muda mrefu bila kuwapeleka Mahakamani.

**44. Mheshimiwa Spika**, imefikia hatua Mawakili na ndugu wa watuhumiwa wa makosa ya mtandao kutoruhusiwa hata kuwapelekea chakula wakiwa mikononi mwa Jeshi hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ya serikali hapa Bungeni kama makosa ya mtandao sasa yametengenezewa utaratibu mpya ambao umekuwa unawatweza na kuwatesa kinyume cha Katiba na sheria za nchi yetu. Taifa linaelekea kuwa la dola la kipolisi kwa sababu ambazo serikali inazijua. Tukiendelea hivi ilivyo, majuto ni mjukuu huja baadae.

## F. HAKI YA KUISHI, HAKI YA HIFADHI YA MAISHA NA UTU IMEWEKWA REHANI

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

**46. Mheshimiwa Spika**, Aidha Katiba yetu inaweka msingi na haki katika ibara ya 14 kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake, **kwa mujibu wa sheria!**. Kwa utaratibu ulivyo sasa haki ya kuishi inaweza kuondolewa kwa utaratibu wa Mahakama; ambapo Tanzania bado inatekeleza adhabu ya kunyonga kwa baadhi ya makosa ya jinai.

**47. Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 4 (2) Katiba inaweka masharti pamoja na mambo mengine kuwa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mahakama ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama vyombo vya utoaji haki nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarejea masharti haya ya Katiba kwa matukio ya utekaji, utesaji, kushambuliwa kwa risasi na kupotea kwa watu nchini inaelekea zipo mamlaka zingine (Kangaroo Courts) ambazo zinahusika na kukamata watu na kuwapa adhabu nje ya mfumo wetu wa utoaji haki.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

**57. Mheshimiwa Spika**, Bunge hili liliwahi kuipatia jukumu mahususi ya kuchunguza hali ya usalama wa nchi, kufuatia shambulio la Mbunge wa Singida Mashariki na malalamiko ya kutishiwa kwa wabunge, Kamati ya Ulinzi na Usalama chini ya Mheshimiwa Rajab Adadi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua matokeo ya uchunguzi huo uliofanywa na kamati ya Ulinzi na Usalama na lini taarifa hiyo itawasilishwa Bungeni kusudi ijadiliwe ili Bunge lifanye maazimio.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

## G. HAKI YA KUPATA DHAMANA NI ZAWADI YA POLISI?

**59. Mheshimiwa Spika**, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 13(6)(b) inatoa katazo na marufuku kwa mtu anayeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo. Aidha ibara ya 13(6)(e) inatoa marufuku kwa mtu yeyote kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza na kumdhalilisha.

**60. Mheshimiwa Spika**, Pamoja na masharti na makatazo hayo ya Katiba kumekuwa na tatizo ambalo linaanza kuwa sugu la kuwachukulia watuhumiwa wakiwa mikononi mwa Polisi na wengine Mahakamani kama vile wameshahukumiwa kuwa wakosaji. Dhamana ni haki ya msingi chini ya kifungu cha 148 cha Sheria ya mwenendo wa Makosa ya Jinai. Tatizo liko katika dhamana ambayo inaruhusiwa kutolewa na Polisi, imekuwa kama ni zawadi kutoka kwa dola kwa sababu ambazo hata hazina mantiki yoyote; wala misingi ya kisheria.

**61. Mheshimiwa Spika**, Mawakili wakiwawakilisha wateja wao mbalimbali wamechukua hatua za kuwasilisha maombi Mahakama Kuu (*Habeas Corpus*) ili kumtaka Inspekta Jenerali wa Polisi kuja mbele ya Mahakama kueleza sababu za kuwashikilia watuhumiwa muda mrefu kinyume cha Sheria. Uzoefu unaonyesha kuwa baada ya Mahakama Kuu kutoa hati ya wito kwa Jeshi la Polisi, siku ya kusikiliza maombi hayo au kabla watuhumiwa wamekuwa wakipelekwa Mahakamani.

**62. Mheshimiwa Spika**, Uharaka wa Jeshi la Polisi kuwapeleka Mahakamani Watuhumiwa baada ya kupata wito wa Mahakama Kuu ni ishara kuwa Polisi hawana sababu wala nia njema ya kuwashikilia Watuhumiwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa huu ni ukiukwaji wa haki wa wazi unaofanywa na maafisa wa Jeshi la Polisi. Utaratibu huu ambao ni kinyume cha Katiba na Sheria wa Jeshi la Polisi umekuwa ukijirudia mara kwa mara na kuonekana kama mazoea na jambo ambalo ni halali mbele yao.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

**64. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulitaka Jeshi la Polisi kutokamata watuhumiwa mpaka pale uchunguzi au upelelezi wao unapokamilika, hii ni kwa sababu kumekuwa na sababu za mara kwa mara zinazotolewa na Mahakama kuwa upelelezi wa shauri fulani la jinai haujakamilika jambo linalopelekea Watuhumiwa wengi kuendelea kusota Magerezani kwa sababu za kutokamilika kwa upelelezi.

## H. JESHI LA POLISI NA MKURUGENZI WA MASHTAKA INAVYOTUMIKA VIBAYA KUMINYA MFUMO WA UTOAJI HAKI NA KUBAMBIKIZIWA KESI ZA UONGO:

**65. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Mashitaka ya Taifa (DPP) imeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo pamoja mambo mengine; inatakiwa kutekeleza mamlaka yake kwa kuzingatia misingi ya kutenda haki, kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki na maslahi ya umma.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

**68. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kwa nini, DPP anachukua muda mrefu kukamilisha upelelezi wa kesi mbalimbali za watuhumiwa wakati akijua kwamba hana ushahidi dhidi ya watuhumiwa kwanini anawakamata na kuwafungulia mashitaka na pengine yasiyo na dhamana, watuhumiwa wa makosa ya mauaji, ugaidi, makosa ya utakatishwaji wa fedha na uhujumu uchumi ni miongoni mwa makosa ambayo mahabusu wanakaa muda mrefu mahabusu, Je, kwa nini sasa sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai pamoja na sheria nyingine zinazohusika zisifanyiwe marekebisho ili

kumwezesha DPP kuwakamata watuhumiwa wakishakamilisha upelelezi wao?

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

**75. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa mwito kwa vyombo vya dola kuhakikisha kuwa hakuna kumkamata mtuhumiwa kama bado hawajafanya uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili kwa sababu kwenye Mahakama zetu zipo hoja ambazo zinajirudia mara kwa mara kuwa uchunguzi bado unaendelea au jalada liko kwa DPP kwa ajili ya uamuzi au jalada lipo kwa Mkemia Mkuu jambo ambalo linasababisha kuchelewesha haki za watuhumiwa.

## I. MASLAHI YA ASKARI WA JESHI LA POLISI

**76. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba upandishwaji vyeo kwa Askari wetu ni moja ya stahiki zao na hufanywa kutokana na sifa na muundo wa Wizara. Hata hivyo sote tunatambua kwamba pamoja na jitihada ambazo zinasemekana zimefanywa lakini yapo malalamiko miongoni mwa Askari wetu ambao wamekaa kipindi kirefu bila kupandishwa vyeo, watu maaskari ambao waliahidiwa kwenda kozi mbalimbali lakini hadi sasa hawajawahi kwenda na huenda tatizo kubwa kama ilivyo kwa kada nyingine ni bajeti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua mpango wa serikali wa kuhakikisha inapandisha vyeo Maaskari wote wenye sifa za kupandishwa vyeo kwa mujibu wa taratibu za Jeshi la Polisi.

**77. Mheshimiwa Spika,** yapo malalamiko pia kwamba, mafunzo kwa Askari kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Jeshi la Polisi zinagharamiwa na Askari wenyewe kwa kukatwa posho zao, badala ya kugharamiwa na mwajiri. Zipo taarifa pia dhidi ya Jeshi la Polisi kutumia fedha nyingi za walipa kodi kwa ajili ya kugharamia mafunzo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwanini hasa Askari wanaokwenda kozi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi, wanakatwa fedha zao za posho ili kugharamia mafunzo hayo?

## J. UHABA WA BAJETI KWA JESHI LA POLISI, NGAZI ZA WILAYA.

**78. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi kirefu sasa yapo malalamiko kutoka kwa wananchi kwenda Jeshi la Polisi kuhusu utoaji wa

huduma. Ukitazama kwa undani utagundua hakuna bajeti kwa ngazi za wilaya, hali hii inasababisha Jeshi la Polisi kukosa hata karatasi za kuandikia loss Report, hakuna hata fomu za PF 3, ni ukosefu wa stationaries ambazo unafanya Jeshi hili kudhaurika na wananchi, kwani wananchi hawa pamoja na kulipa kodi lakini wanalazimika kuchangia mafuta magari ya Polisi, kuambiwa watoe nakala za karatasi/ fomu kulingana na shida ya mwananchi. Miaka zaidi ya hamsini baada ya uhuru, Tanzania bado tunakosa hata fomu za PF3 kwenye vituo vyetu vya Polisi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuongeza na kupeleka Bajeti kwa Ngazi za Wilaya na Vituo vya Polisi kuliko utaratibu wa sasa.

## K. UTARATIBU WA KUACHA KAZI.

**79. Mheshimiwa Spika,** zipo taarifa kwamba katika utendaji na utumishi wa Jeshi la Polisi, upo utaratibu ambao unawaruhusu Askari kutokana na sababu mbalimbali kuacha kazi, hata hivyo taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imezipata ni kwamba, kwa sasa baadhi ya Maaskari wanaoomba kuacha kazi wanazuiliwa. Taarifa zaidi zinasema upo waraka ambao umetolewa kwenda kwa Ma RPC nchini kuwakataza kusaini maombi ya barua za maaskari wanaoomba kuacha kazi kwa sababu mbalimbali. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, misingi ambayo imewekwa kwa mujibu wa Police General Order izingatiwe.

## L. UFISADI NA MATUMIZI MABAYA YA FEDHA ZA UMMA KWA JESHI LA POLISI.

### (a) UFISADI KATIKA UNUNUZI WA MAGARI 77 YA JESHI LA POLISI

**80. Mheshimiwa Spika**, zipo taarifa kwamba Jeshi la Polisi linatuhumiwa kupokea magari yenye thamani za 10,362,135 ambayo ni sawa na shilingi 23,221,544,535 kutoka kwa mzabuni M/S Ashok Leyland Limited na hata hivyo inaonekana kuwepo na upungufu kwa kiasi kilichoingizwa katika vitabu vya fedha na hivyo inaonekana kukiwa na upungufu wa kiasi cha fedha zaidi ya Bilioni 23.

## (b) UFISADI KATIKA UNUNUZI WA SARE ZA JESHI LA POLISI

**81. Mheshimiwa Spika**, zipo taarifa kwamba Jeshi la Polisi Tanzania linatuhumiwa kufanya manunuzi ya sare za Jeshi la Polisi zenye thamani ya shilingi Billioni 16,660,000,000.00 lakini katika hali ya kustaajabisha hakuna ushahidi wowote wa uagizwaji na upokeaji wa sare hizo kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi. Pamoja na hilo, Jeshi la Polisi linalalamikiwa kwa kutozingatia ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu uwasilishaji wa Kiapo cha Nguvu ya Kisheria (Power of Attorney) na leseni halali ya biashara. Aidha taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo zinaonesha kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani wakati wa kusaini Mkataba hakuzingatia ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hata hivyo katika hali ya kushangaza zaidi Jeshi la Polisi lililipa jumla ya Sh. 16,660,000,000 bila ya kuwa na ushahidi wa uagizaji na upokeaji wa Sare za Polisi kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi.

**82. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitarajia kuwaona wahusika hawa wakipelekwa kwenye mahakama ya mafisadi na au kukabiliana na mashitaka ya matumizi mabaya ya Ofisi pamoja na makosa ya uhujumu uchumi na badala yake wahusika wako mitaani na wanaendelea kura raha, huku serikali ikishindwa kuwachukulia hatua,

## (c) UFISADI KATIKA UJENZI WA VITUO VYA POLISI

**83. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazotaarifa za ujenzi wa vituo vitatu vya Polisi katika mkoa wa Singida kwa gharama ya shilingi, 592,990,000 kinyume na Mpango kazi kati ya Jeshi la Polisi na wafadhili. Kwa mujibu wa mpango kazi na wafadhili ilikubaliwa kwamba kujenga au kurekebisha kituo kimoja katika kila Mkoa lakini kwa sababu ambazo hazikujulikani vituo vyote 3 vilijengwa mkoa mmoja na kunyima fursa mikoa mingine kupata huduma hiyo. Kitendo hiki ni cha ki binafsi zaidi kuliko kupeleka huduma kwa wananchi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara yenye dhamana kuliambia Bunge lako Tukufu sababu za kujengwa kwa vituo vitatu vya mfano mkoa mmoja tofauti na makubaliano na wafadhili.

## HAKI ZA MAHABUSU NA WAFUNGWA WALIOKO MAGEREZANI

**84. Mheshimiwa Spika,** katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka (1977), Ibara ya 13(6)(c)(d) inazungumzia

kwa kina kuhusu haki za raia wote bila ubaguzi wowote . Katika Ibara ndogo ya sita inatoa ***marufuku kwa mtu yoyote kuadhibiwa kwa sababu ya kitendo chochote ambacho alikitenda hakikuwa ni kosa chini ya sheria, na pia kwamba ni marufuku kwa adhabu kutolewa ambayo ni kubwa kuliko adhabu iliyokuwepo wakati kosa linalohusika lilipotendwa.*** Ibara hii pia inazungumzia haki na usawa wa binadamu ambapo ***heshima ya mtu itatunzwa katika shughuli zote za upelelezi ambapo mtu huyo atakuwa chini ya ulinzi bila uhuru***.

**85. Mheshimiwa Spika**, Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika mahabusu na magereza zetu nchini. Tatizo kubwa sio kwa waliopewa dhamana za kuwasimamia wafungwa magerezani bali kwa sababu ya mfumo kandamizi wa vyombo vya utoaji haki nchini vinavyopokea maelekezo nje ya mfumo wa Magereza.

**86. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuwa magereza zetu nchini zina msongamano mkubwa sana wa wafungwa jambo ambalo ni hatari kubwa kwa afya za wafungwa. Lakini pia ndani ya magereza kuna wafungwa wengi ambao wamefungwa muda mrefu kwa makosa madogo madogo na hivyo kusababisha msongamano huo pasipo ulazima wowote. Mfano, zipo kesi za wafungwa waliokutwa wakiiba chakula, waliogombana na kupigana mitaani, waliokutwa wamelewa, wanaotuhumiwa kuwakosoa viongozi wa nchi mitandaoni au kwenye mikutano ya hadhara n.k.

**87. Mheshimiwa Spika,** katika Ibara 13 (6) Katiba yetu inakataza kutolewa kwa adhabu kubwa kuliko adhabu iliyokuwepo wakati kosa linalohusika lilipotendwa. Jambo la kushangaza ni kuwa makosa haya madogo madogo yamekuwa yakiwaweka watu wengi mahabusu kwa muda mrefu jambo ambalo ni kinyume kabisa na matakwa ya kikatiba. Yapo makosa mengi yanayofanywa katika jamii ambayo yanaweza kabisa kurekebishika bila watuhumiwa kufikishwa mahabusu au magerezani lakini kutokana na mifumo mibovu ya utoaji haki vijana wengi ambao ndio nguvu kazi ya taifa wameishia magerezani.

**88. Mheshimiwa Spika**, Pamoja na hilo katika mfumo wa utendaji kazi ndani ya jeshi la polisi pameibuka tabia inayozidi kushamiri nchini kwa sasa ambapo yapo mambo yanayotajwa na

polisi kama makosa ya kisheria ila kwa uhalisia sio makosa ya kisheria.

**89. Mheshimiwa Spika,** wapo vijana wengi wamewekwa mahabusu kwa *kueleza fikra zao na kutoa maoni* dhidi ya mwenendo wa viongozi waliowapa dhamana ya kuongoza serikali. Jambo la kushangaza ni kuwa haki hiyo ya kutoa maoni inavishwa taswira ya uchochezi au ukosoaji. Vijana wengi wamejikuta mikononi mwa vyombo vya dola wengi wao wakitupwa mahabusu au magerezani kwa kutumia haki yao ya kueleza fikra zao ambayo ipo kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi. Jambo hili sio tu kwamba linazidisha msongamano usio wa lazima katika magezera bali pia ni hatari kwani linatengeneza tabia za usugu hususani kwa vijana wadogo walio kwenye magereza hizo.

**90. Mheshimiwa Spika,** Mwanasaikolojia Christian Jarrett katika kitabu chake cha "on the dark underbelly" anaeleza kwa kina madhara yanayoweza kutokea endapo mrekebishaji wa tabia atatumia njia isiyo sahihi katika kurekebisha tabia fulani ya mwanadamu. Kitendo cha kuendelea kuwaweka mahabusu watuhumiwa wenye makosa madogo madogo kunazalisha matatizo makubwa sio tu kwa mtuhumiwa bali kwa jamii kwa ujumla na kufanya Magereza na Polisi kuonekana kama sehemu za kawaida na hivyo kuhamasisha wahalifu wengine katika Nyanja zingine kujenga dhana kuwa Magereza ni sehemu za kawaida za kuishi.

**91. Mheshimiwa Spika**, Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha kuwa inapunguza msongamano kwenye mahabusu na magerezani kwa kutumia adhabu mbadala ya vifungo vya nje au kazi za kijamii. Pia, serikali hii ya awamu ya tano iache mara moja kuendelea kuwashikilia vijana mahabusu au kwenye magereza eti kwa makosa ya kuzungumza fikra zao au kutoa maoni dhidi ya mienendo ya viongozi wa serikali. Ni lazima serikali itambue kuwa haki hii ipo kikatiba na ni lazima serikali iheshimu na kulinda katiba ya nchi kwa kuwa hakuna mtu yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye mamlaka yoyote *juu* ya katiba ya nchi.

## M. ASKARI WA USALAMA BARABARANI NA DHANA YA KUWA IDARA YA TRA

**92. Mheshimiwa Spika**, Kwa nyakati mbalimbali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikihoji namna Jeshi la Polisi kitengo cha Usalama Barabarani kilivyogeuka kuwa mamlaka ya kutoza mapato badala ya kusimamia usalama kwa watumiaji na wamiliki wa vyombo vya moto, Pamoja na matamko na maelekezo ambayo Waziri mwenye dhamana ameyatoa lakini Askari wa Usalama Barabarani bado wanaonekana dhamira yao kubwa ni kupata mapato.

**93. Mheshimiwa Spika**, ilitarajiwa msisitizo kuwa Askari wa Usalama Barabarani kutoa elimu ya usalama barabarani na kuonya kuhusu makosa madogo madogo barabarani, lakini hali ni tofauti kwa sababu wananchi wengi wanalalamika badala ya kupewa elimu ya usalama barabarani wamekuwa wakitozwa fedha za faini ya makosa ya barabarani ambayo hayahitaji kupigwa faini zaidi ya kupewa elimu ya kawaida.

**94. Mheshimiwa Spika**, Taarifa kutoka kwa wadau mbalimbali ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo zinaonesha kwamba, upo utaratibu ambao Askari hupewa na au hupangiwa kiwango cha fedha ambacho anapaswa kukusanya kwa siku, na asilimia fulani ya fedha hizo kuwa ni kamisheni yake jambo ambalo linajengewa hoja kuwa faini za barabarani ni chanzo kimojawapo cha mapato.

**95. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haiungi mkono uvunjwaji wa sheria za usalama barabarani na wala haijengi hoja ya wakosaji kutoadhibiwa kwa mujibu wa sheria hizo, lakini cha kushangaza ni pale Askari wa Usalama barabarani wanapotoza faini hata kwa makosa ambayo hayapo kwa mujibu wa sheria. Mathalani kuweka mizigo kwenye siti ya abiria kwa gari binafsi jambo ambalo halipo kwa mujibu wa sheria ya usalama barabarani.

**96. Mheshimiwa Spika**, Faini za Usalama barabarani zinaweza kuleta chuki katika jamii kwa sababu ya hisia zinazojengeka kuwa wamiliki wa magari ni watu wenye fedha kwa hiyo ni haki yao kutozwa faini kwa jinsi mtu yeyote anavyojisikia. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa hili sio jambo la kufumbia macho kwa sababu linaweza kuhatarisha amani na utulivu katika taifa.

## N. IDARA YA UHAMIAJI

**97. Mheshimiwa Spika**, Idaya ya Uhamiaji nayo kama ilivyo kwa Jeshi la Polisi hapa nchini imekuwa ikifanya kazi kwa maelekezo ya wanasiasa hali inayoshusha hadhi ya kiweledi kwa idara hii. Yapo matukio ambao yamefanywa na Idara hii na kuacha maswali mengi ndani na nje ya jamii ya watanzania.

**[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

**103. Mheshimiwa Spika**, Idara ya Uhamiaji Fungu 93 kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo hali ni mbaya sana na kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Uhamiaji kwa kipindi cha Julai hadi Februari 2019, inaonesha Idara ilikuwa imetengewa jumla ya Shilingi 10,000,000,000.00 kwa ajili ya shughuli za maendeleo lakini hadi kufikia mwezi Februari, Idara ya Uhamiaji haikupata hata shilingi moja.

**104. Mheshimiwa Spika,** kutokana na Serikali hii ya awamu ya tano kushindwa kupeleke fedha za maendeleo, kunaleta sintofahamu kuhusu miradi ambayo ilikusudiwa kutekelezwa kwa kutumia fedha hizo, hadi sasa Miradi ya Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji Mikoani, ikiwa ni pamoja na kuanza Ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji Dodoma, Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi, Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Geita, Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara, Mradi wa kukamilisha Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara, Mradi wa kumalizia ujenzi wa nyumba ya Kamishina Jenerali wa Uhamiaji Masaki- Dar es Salaam, Mradi wa kukamilisha ukarabati wa Nyumba Makazi ya Watumishi Ibinzamata Mkoani Shinyanga, Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Simiyu, Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Songwe na Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Katavi, Miradi hii yote haikupata hata shilingi moja na imesimama kutokana na ukosefu wa fedha.

**105. Mheshimiwa Spika**, wakati miradi hiyo ikishindwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 taarifa ya makadirio ya mapato, matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Fungu 93 inaonesha Idara ya Uhamiaji haijapangiwa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kushindwa kupangiwa fedha za Maendeleo kwa Idara hii, kwa maneno mengine ni kuendelea kutelekeza miradi

mbalimbali ya ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika mikoa mbalimbali ambayo imeorodheshwa hapo juu.

**106. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutolea ufafanuzi jambo hili, Ni kwa nini Serikali imeshindwa kupeleka hata shilingi moja kwenye miradi ya ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji maeneo mbalimbali nchini kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Pia Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 haijatenga kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya kukamilisha Miradi ya Ujenzi wa Ofisi mbalimbali ambazo zimetelekezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 ikiwemo miradi ya Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Simiyu, Songwe na Katavi iliyotarajiwa kuanza kujengwa?

**107. Mheshimiwa Spika**, Idara ya Uhamiaji inazochangamoto nyingi ambazo Serikali hii kama ilivyo kwa sekta nyingine imeshindwa kuzitatua, hadi sasa kwa taarifa zilizopo za mwaka 2012, miaka 7 nyuma Idara ya Uhamiaji ilikuwa inahitaji watumishi 10,000, hadi sasa idadi hii lazima imeongeza kulingana na mazingira ya sasa. Kati ya watumishi 10,000 waliokuwa wanahitaji, watumishi waliopo ni 2,838 na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 7,162. Kwa hali Mheshimiwa Spika, tunatarajia muujiza gani wa ufanisi katika Idara hii nyeti?

**108. Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa sababu za msongamano wa magereza yetu hapa nchini ni kuwepo kwa wahamiaji haramu ambao wanashikiliwa katika magereza mbalimbali hapa nchini. Kwa takwimu zilizopo jumla ya wahamiaji haramu 3,260 wanashikiliwa hapa nchini baada ya kumaliza vifungo vyao, Kambi Rasmi inataka kujua Serikali ina mkakati gani kuhakikisha wahamiaji hao ambao wanatoka katika nchi za Ethiopia, Burundi na Rwanda watarejeshwa kwao na kulipunguzia gharama Taifa za kuendelea kuwatunza katika magereza zetu na kupunguza msongamano magerezani kwa kuwa wameshamaliza vifungo vyao!

**109. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua pia ni lini Serikali italipa madeni ya watumishi na wazabuni katika Idara ya Uhamiaji ambayo yanafikia sasa kiasi cha Sh. 6,470,223,842.83? Aidha Serikali ina mpango gani kuhakikisha matatizo kama ya sare na vitendea kazi yanamalizwa kwa uharaka, ni aibu miaka zaidi ya hamsini tangu kupata uhuru Taifa

linakuwa na changamoto ya uhaba wa sare kwa Idara nyeti kama ya Uhamiaji.

## O. MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)

**110. Mheshimiwa Spika,** tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa hadi sasa ni idadi ndogo sana ya watanzania ambao wameshapatiwa vitambulisho hivyo, inavyoelekea ni kama kasi ya kupatiwa vitambulisho vya mjasiriamali ni kubwa kuliko Vitambulisho vya Taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua tatizo la NIDA ni kitu gani hasa, Kwa taarifa ambazo siyo rasmi inaonekana kwamba Rasilimali na fedha havitoshi ukilinganisha na matokeo yanayotarajiwa. Ni lini Serikali itaongeza Rasilimali watu na Fedha ili kuharakisha mchakato wa kuwapatia vitambulisho vya uraia watanzania kwa wakati?

**111. Mheshimiwa Spika,** hata hivyo kuna taarifa kwamba kasi ya uzalishaji wa vitambulisho vya taifa ni ndogo na kati ya watu 19,662,105 waliojiandikisha ni kadi 4,511,809 tu za vitambulisho ndo zimetengenezwa na idadi hii ni sawa na 23% ya idadi ya watu walioandikishwa. Pamoja na hali kuwa hivi, tunaona matangazo ya kusajili laini za simu za Mkononi kwa mfumo wa alama za vidole na ili usajiliwe lazima uwe na kitambulisho cha Taifa na ikiwa kasi yenyewe ndiyo hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka watanzania wafanye nini katika hali hii, na wakati huohuo Mkandarasi ambaye amesimamisha kazi kutokana na serikali kushindwa kumlipa jumla ya deni la $ 30,175,107,600/=

**112. Mheshimiwa Spika,** kuwafungia watanzania mawasiliano kwa sababu ya kushindwa kusajili laini zao kwa kukosa Vitambulisho vya Taifa siyo kuwatendea haki, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inasuasua na wapo wananchi wengi walioomba vitambulisho kwa kipindi kirefu sasa, lakini hadi sasa hawajapatiwa vitambulisho hivyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulitolea ufafanuzi jambo hili ambalo limezua sintofahamu kwa watanzania, hasa kuhusu lini hasa watanzania ambao walishakamilisha zoezi la kuomba vitambulisho hivyo watavipata na utaratibu wa matumizi ya vitambulisho hivyo kwa wale ambao hawajavipata dhidi ya zoezi jipya la usajili wa namba za simu za mikononi.

## P. UFISADI MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)

## Q. HALI MBAYA YA UCHUMI NA TISHIO LA USALAMA NCHINI

**113. Mheshimiwa Spika**, Ukweli usiopingika ni kwamba, upo uhusiano wa karibu kati ya uchumi na usalama wa nchi, na kwa bahati mbaya sana kama Taifa hatujafanya vizuri katika diplomasia ya uchumi, hali hii imesababisha kada za wafanyabiashara na wawekezaji kuwa miongoni mwa kada ambazo ziko katika wakati mgumu kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo, urasimu wa mifumo ya usimamizi wa taasisi za serikali na hivyo kupelekea kero kubwa sana kwa wafanyabiashara. Pamoja na mambo mengine kama Taifa linakabiliwa na athari zinazotokana na kuzorota kwa biashara ambazo zinasababisha ukosefu wa ajira. Kila mwaka takribani vijana zaidi laki 7 hawawezi kuendelea na masomo ya elimu ya juu na kimsingi ukuaji mzuri wa biashara na uwekezaji ungeweza kuwahakikishia vijana hawa ajira ambazo hazihitaji utaalam wa hali ya juu.

**114. Mheshimiwa Spika**, Kwa sasa baadhi ya wawekezaji wamefunga uwekezaji wao na baadhi ya wafanyabiashara wamefunga maduka yao na sehemu zao za biashara, na ni wazi kila mtanzania anaona namna ambavyo wawekezaji wanakimbia na kuhamisha mitaji, biashara za kati na za juu zinafungwa, watanzania wanakosa ajira jambo ambalo siyo tu kwamba linasababisha ajira kukosekana, lakini tishio kubwa ni usalama wa nchi hasa kwa kundi la vijana ambalo linazidi kukosa ajira na hivyo kutishia ongezeko la uhalifu nchini.

**115. [MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazotaarifa ya vikosi kazi vilivyoundwa kwa kushirikiana na baadhi ya taasisi za fedha ambazo wamekuwa wakitoa taarifa za wateja wao kwamba wanaviwango fulani vya fedha katika akaunti zao. Tishio zaidi linakuja pale ambapo akaunti za mwananchi hufungwa na kutakiwa kutoa kiasi cha fedha kwa madai ya kwamba anadaiwa kodi, Matukio ya namna hii dhidi ya mali za watanzania katika Taifa lao na yenye sura ya uporaji lazima yakome na Serikali ihakikishe inakusanya Kodi yake halali.

## R. HITIMISHO

**116. [MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEZO YA KITI]**

**117. Mheshimiwa Spika**, Bunge hili kwa niaba ya wananchi wa Tanzania linaowajibu wa kuisimamia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tunatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kutekeleza wajibu wetu kikamilifu, Serikali hizi zinakuja na kupita kama zilivyopita awamu nyingine, Taifa hili litabaki, tutumieni nafasi yetu kulinda Taifa hili.

......................................

David Ernest Silinde (Mb)

Kny: **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

24 Aprili, 2019